

KUFUKUZA MPANGAJI NA UFUNGUZI WA MAHAKAMA:

Miliki wa nyumba yangu aliwasilisha ombi la kunifukuza. Ni nini kitakachofuata?



Utapokea tarehe ya kesi yako ana kwa ana au itawekwa kwenye nyumba yako
**IKIWA PESA YOTE INAYODAIWA + ADA YA MAHAKAMANI ITALIPWAKABLA YA UAMUZI KUFANYWA
, KESI YA KUHAMISHWA INAPASWA KUFUTILIWA MBALI.**

Ninaweza kumpigia nani simu kupata msaada wa Kisheria?

Laini ya simu ya EHOCS ya Kufukuza Mpangaji Hotline: 314-534-5800

Huduma ya Kisheria ya Missouri ya Mashariki: 314-534-4200

Arch CityDefenders: 314-361-8834

St. Francis CLAM: 314-977-3993

Mradi wa Haki ya Makazi ya Wahamiaji : 314-256-5980

Nimechelewa kulipa kodi ya nyumba...

- ♦ **Wasiliana na United Way: Bonyeza 2-1-1**
Zungumzia mpango wa malipo na mwenye nyumba wako
- ♦ **Ratibu mapatanisho na mwenye nyumba yako**
(STL City) Kituo cha Kusuluhisha Mzozo : 314-255-7449
(STL County) Mradi wa Mapatanisho ya St. Louis : 314-833-0226

Jinsi ya kupata habari kuhusu kesi yako.

Tarehe ya kesi yako italetwa moja kwa moja au itawekwa kwenye mlango wako. Unaweza kupata tarehe ya kesi yako kwenye CaseNet (courts.mo.gov)

- ↳ Tafuta jina lako la kwanza na la mwisho kwenye Casenet (jaribu herufi zote zinazoweza)
- Hakikisha anwani sahihi ya katikati, anwani ya kesi na mwaka uliowasilishwa
- ↳ Baada ya kubofya jina lako, chagua tabo ya "hearings and trials" kuona tarehe ya kesi yako ikiwa hauna intaneti kwa ajili ya kesi, watetezi wa jamii huenda wakaweza kukusaidia k.v maktaba ya eneo lako au kituo cha jamii
- ↳ Ikiwa tarehe yako ya kesi imepita, tazama tabo ya the "Civil Judgements" kwa maelezo zaidi

Ni nini hufanyika katika kesi?

- ♦ Mwenye nyumba wako huenda akawa tayari kusuluhisha kesi na wewe kabla ya kesi, kwa kufanya mpango wa malipo. **Huhitajiki kamwe** kufikia mapatano kwa kesi yako ikiwa hautaki. Ikiwa mtapatana, hautakuwa na kesi mbele ya hakimu.
- ♦ Mwenye nyumba wako huenda akakuomba utie sahihi mkataba unaoitwa "Idhini ya Uamuzi". Idhini ya uamuzi bado ni uamuzi wa kufukuzwa na itaoneka kwenye rekodi yako.
- ♦ Idhini ya uamuzi inapaswa kusema kiasi cha pesa mwenye nyumba wako anakudai, na ikiwa unakubali kuhama kufikia tarehe hususa. Soma mkataba kwa makini na **utie sahihi tu ikiwa unakubaliana nao.**
- ♦ Ikiwa haukubaliani nao, una haki ya kuomba mwendelezo au kuomba tarehe ya kesi.
- ♦ Unapaswa kuhudhuria kesi **zote** kuepuka hukumu chaguomsingi katika kesi hii.
- ♦ Hukumu chaguomsingi inamaanisha uamuzi utampendelea mwenye nyumba.

Kesi yako itaenda mahakama ni wakati gani?

- ♦ Mpangaji ana haki ya kuomba kusikilizwa mahakamani **badala** ya kutia sahihi idhini ya uamuzi.
- ♦ Ikiwa kuna mzozo kuhusu kiasi kinachodaiwa, hakikisha umekuja na risiti au stakabadhi ya kuunga mkono madai yako kwenye kesi.
- ♦ Unaweza kuomba mwendelezo kwa wakati zaidi kukusanya stakabadhi zinazohitajika.

Tazama ukurasa unaofuata kwa habari zaidi kuhusu utaratibu wa mahakamani kwa ajili ya kesi.

Kwa Habari zaidi wasiliana na: Metropolitan St. Louis Baraza la Nyumba na Fursa Sawa(EHOC)

Tovuti: www.ehocstl.org
Simu: 314-534-5800

f :@ehocstl
t :@ehocstl

KUFUKUZA MPANGAJI NA UFUNGUZI WA MAHAKAMA:



Miliki wa nyumba yangu aliwasilisha ombi la kufukuzwa. Ni nini kitakachofuata?

Kabla ya kufika mahakamani, tafuta kujua ikiwa mwenye nyumba yako anawakilishwa na wakili



Jinsi gani? Mwenye nyumba wako hajawakilishwa ikiwa unaishi jiji la St. Louis na tarehe yako ya mahakamani ni **Ijumaa** saa 3:30 Asubuhi, au ikiwa unaishi Kaunti ya St. Louis na tarehe yako ya mahakamani ni Jumanne saa 7 Alasiri.



Kwa nini? Ikiwa mwenye nyumba wako hajawakilishwa, mara yako ya kwanza kufika mahakamani huenda ikawa kesi, na unahitaji kuja ukiwa tayari na majibu yaliyojazwa awali ili kujitetea. Ikiwa mwenye nyumba wako ana wakili, tarehe ya kesi itawekwa mara ya kwanza kufika mahakamani.



Hakimu anatoa uamuzi kuhusu kufukuzwa

Hakimu anafanya uamuzi unaompendelea mwenye nyumba

Hukubaliani na uamuzi? Tuma maombi ya kesi mpya ndani ya siku 10

Mwenye nyumba anaweza omba askari akuhamishe baada ya siku 10

Hakimu anafanya uamuzi unaompendelea mpangaji

Mpangaji analipa pesa zote anazodaiwa ndani ya siku 10 na anaendelea kuka

Kesi ya kufukuzwa imefutuliwa mbali

Mkataba au uamuzi wa idhini unafanywa kati ya mpangaji na mwenye nyumba

Mpangaji anafuata masharti ya mkataba

Mpangaji hafuati masharti

Mwenye nyumba huenda akaomba uhame au pesa ya marekebisho

Kituo cha kuthibiti Magonjwa (CDC) ilisitisha kufukuzwa kwa baadhi ya wapangaji wanaostahili kitaifa kuanzia Septemba 4 hadi Desemba 31, 2020.

Kwa habari zaidi tembelea: <https://tinyurl.com/y5rdv4vy>